

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MRADI WA
UPIMAJI NA UZAJI VIWANJA-DODOMA MANISPAA
13 APRILI 2018.**

I.UTANGULIZI

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. **Dr John Joseph Pombe Magufuli** alivunja Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu CDA kwa Tangazo/Tamko kupitia Gazeti la Serikali Na. 213 la tarehe 15 Mei, 2017, Baada ya tamko hilo Majukumu yote ya iliyokuwa CDA yalikabidhiwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kuanzia mwezi Julai mwaka 2017.

Halmashauri ya Manispaa Dodoma ilianza kujipanga kwa utekelezaji wa shughuli zote ambazo zilikwisha kukamilika na ambazo hazidakamilika na kubuni miradi mipya kwa kazi na majukumu yake kama ifuatavyo;

- i) Uandaaji Mipango Kina (Detailed Planning Scheme),
- ii) Upimaji wa Viwanja (Surveying),
- iii) Uandaaji ramani na Hati (Deed plans),
- iv) Utoaji wa hati milki za Ardhi (Title Deed),
- v) Ubadilishaji Ground Lease kuwa Hati milki ya miaka 99,
- vi) Utatuzi wa migogoro,
- vii) Utoaji vibali vya ujenzi,
- viii) Udhibiti Ujenzi Holela na
- ix) Umilikishaji mpya wa ardhi.

Mpango wa Upimaji wa viwanja kwa kipindi cha mwezi Januari, 2018 hadi Disemba, 2018 ni kupima viwanja laki moja (100,000), hadi sasa viwanja 13,464 vmeshapimwa na kukamilika kwa mchanganuo ufuatao Iyumbu (967), Mtumba (10,000), Michese (1,500) na Nala (7,000).

Viwanja 10,864 vilivyopo eneo la Mtumba na Iyumbu vimekamilika na uuzaji wake utanza tarehe 20/04/2018, viwanja 2,600 vipo kwenye hatua za ukamilishwaji na vitaingia sokoni kabla ya tarehe 28/04/2018.

Pia Halmashauri imeendelea na Mpango wa Upimaji wa maeneo ya viwanda kwenye maeneoya Mpunguzi, Nala, Nzasa, Chihanga, Hombolo, Ipagala na Mbabala.

Bei za Viwanja zitakuwa kama ifuatavyo kwa mita moja ya mraba:

ENEO LA MTUMBA (UKANDA WA BARABARA YA LAMI)

- Makazi 8,000/=
- Makazi na Biashara 8,500/=
- Biashara 10,000/=
- Taasisi 7,000/=
- Viwanda vidogo 20,000/=

UKANDA WA KATI

- Makazi 6,000/=
- Makazi na Biashara 7,500/=
- Biashara 8,000/=
- Taasisi 5,000/=
- Viwanda vidogo 15,000/=

UKANDA WA BARABARA YA KIKOMBO

- Makazi 3,000/=
- Makazi na Biashara 5,500/=
- Biashara 6,000/=
- Taasisi 5,000/=
- Viwanda vidogo 10,000/=

ENEO LA IYUMBU

- Makazi 6,000/=
- Makazi na Biashara 8,000/=
- Biashara 15,000/=
- Taasisi 7,000/=
- Viwanda vidogo 20,000/=

Mauzo ya Viwanja yatafanyika kuanzia tarehe 20.04.2018. Utaratibu wa mauzo utakuwa kama ifuatavyo:

Kwa wananchi walioomba viwanja Manispaa watafika kwenye eneo la ofisi za zamani za Halmashauri na kuhakiki majina yao ambayo yatakuwa yamebandikwa kwenye mbao za matangazo. Ni lazima mwananchi afike na kitambulisho cha kumtambulisha. Kabla ya kuchagua kiwanja mwananchi anatakiwa kulipa Tshs. 20,000/= za fomu.

Mwananchi akishachagua kiwanja atapewa hati ya madai ya kiwanja hicho na kutakiwa kulipa fedha zote ndani ya siku Thelathini (30) tangu tarehe uliyopokea hati ya madai.

Kwa watumishi wa Umma wanaohamia Dodoma watapelekewa hati ya madai kupitia Makatibu Wakuu wa Wizara zao na watatakiwa kufanya malipo ndani ya siku Thelathini (30).

Naomba kuwasilisha.



Godwin E. Kunambi

**MKURUGENZI WA MANISPAA
DODOMA**